Mwananchi, Jumapili Septemba 14, 2025 Pg 6

UCHUMI

# Faida, hasara mabasi ya kusafirisha abiria wa SGR

Nasra Abdallah, Mwananchi
nabdallah@mwananchi.co.tz

**Dar es Saalam.** Kampuni ya mabasi ya Faima imetambulishwa rasmi na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kama mshirika wa kusafirisha abiria wa treni ya kisasa ya umeme (SGR) mikoa ya Dodoma na Morogoro, hatua iliyoibua mitazamo tofauti kutoka kwa wadau wa sekta ya usafirishaji kuhusu ufanisi na athari za huduma hiyo.

Utambulisho wa kampuni hiyo ulifanyika jana mbele ya waandishi wa habari, ambapo TRC ilieleza, yataanza kutoa huduma kuanzia Septemba 15 kwa kuwachukua abiria wanaoshuka kwenye vituo vya Morogoro (Stesheni ya Jakaya Kikwete) na Dodoma (Stesheni Kuu Samia Suluhu Hassan), pamoja na kuwapeleka stesheni wakati wa kusafiri kwa treni ya SGR.

Ambapo kwa Mkoa wa Morogoro yatatoa huduma ya usafiri kutoka Stesheni ya Jakaya Kikwete kwenda vituo vya Viwandani, Stendi ya Mabasi Msamvu, Masika na stendi ya zamani ya mabasi.

Kwa Jiji la Dodoma yatatoa huduma ya usafiri kati ya Stesheni Kuu ya Samia Suluhu Hassan na kituo cha mabasi cha Nanenane, Machinga Complex na Shoppers Plaza na katika safari zote hizo nauli itakuwa ni Sh5,000.

**13**

**Idadi ya mabasi yatakayokuwa yakitoa huduma ya kusafirisha abiria kutoka stendi ya SGR Morogoro na Dodoma.**

Akizungumzia huduma ya mabasi hayo, Kaimu Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Maendeleo ya Biashara wa TRC, Frederick Massawe alisema ushirikiano huo ni sehemu ya mkakati wa TRC wa kuboresha huduma za reli kwa kuzifanya kuwa jumuishi, bora, na zinazohusisha ushirikiano na sekta binafsi.

Mkurugenzi wa Fahima, Ceaser Amin alisema katika utoaji huduma hiyo watakuwa na mabasi 13, saba yatahudumia Dodoma na sita Morogoro, ambapo yapo yanayochukua abiria 30 hadi 50 na watasafirisha abiria 472 kwa wakati mmoja kwa Dodoma na abiria 180 kwa Morogoro.

Katibu wa Chama cha Taxi Mtandao, Nobel Ford alisema hilo lina faida na hasara kwao kwa sababu inaenda kutoa huduma kwenye mikoa ambayo wao wapo pia, lakini kuna faida kwa abiria kwani gharama ipo chini ukilinganisha na wanayotoza wao.

"Kutoka Stesheni Kuu ya Samia Suluhu Hassan kwenda stendi ya Nanenane sio chini ya Sh12,000 kwa gari (taksi mtandao)." Kuhusu hasara amesema watathirika kwani kuna uwezekano abiria wakapungua, ila Serikali itaathirika pia kwa kupungua mapato kutoka kwa watoa huduma wengine ikiwamo taksi.

Mwenyekiti wa Chama cha Bodaboda na Bajaji Mkoa wa Dodoma, Chacha Marwa alisema kwa faida anaona abiria watakuwa na uhakika wa kusafiri salama zaidi ukizingatia wengine huingia usiku, lakini pia kuepuka kuchelewa kwa kuwa mabasi hayo yatakuwa yanaenda kwa muda. "Ukiacha faida hizo lakini pia ni utekelezaji wa ule wimbo wa kuzalisha ajira nchini hapa sasa utakuwa unafanyika kivitendo," alisema Marwa.

Alishauri pamoja na faida hizo ni vema kukawa na utaratibu wa maegesho kwa mabasi hayo, bodaboda na bajaji ili abiria awe na uhuru wa kuchagua anataka kusafiri na chombo kipi.

Mwenyekiti wa bodaboda na bajaji Mkoa wa Morogoro, Paul Sinya alisema ujio wa usafiri huo kwao sio tishio, kwa kuwa hata taksi mtandao zilivyoanza ziliwakuta na wanaendelea kufanya nao kazi hadi leo.

Alisema bado usafiri wa boda na bajaji unahitajika, kwani hata katika vituo vilivyotajwa kuwa vitashusha abiria sio mwisho wa safari, wapo wanaoingia ndanindani hivyo lazima watahitaji huduma yao tu, lakini pia wasiotaka kukaa kwenye foleni barabarani.

"Nauli ya bodaboda au bajaji huwezi kuilinganisha na ya usafiri mwingine, pia ni wa haraka ukipanda mnaondoka haina kusubiriana," alisema.

Ashura Badi, mkazi wa Dodoma na John Abdallah wa Dar es Salaam, wakisema utarahisisha safari na kuongeza usalama, unafuu kwa wanaotaka kuunganisha safari ambapo watapelekwa stendi kuu za mabasi.



Abiria wakishuka katika treni ya SGR jijini Dodoma. Picha Maktaba

## TAHARIRI /WAZO/NUKUU/MSAMIATI

Habarileo Jumapili

# Hongera TRC kwa ubunifu wa huduma SGR

KATIKA gazeti letu la leo kuna habari isemayo: 'Abiria SGR Dodoma, Moro kufikishwa vituoni kwa basi.'

Vyanzo vya habari ni Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Faima, Ceaser Amin na Kaimu Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Maendeleo ya Biashara wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Frederick Massawe.

Kwa mujibu wa habari hiyo, TRC imetangaza rasmi ushirikiano kati yake na Kampuni ya Faima iliyopewa jukumu la kusafirisha abiria kwa mabasi kutoka stesheni za Reli ya Kisasa (SGR) Dodoma na Morogoro kwenda katika vituo mbalimbali katika miji hiyo.

Huduma hizo zinatarajiwa kuanza kesho na ni matokeo chanya ya serikali kutoa nafasi kwa sekta binafsi kuangalia fursa zilizopo katika huduma ya uwepo wa treni za SGR na kuzichangamkia.

Hii inalenga kutoa na kuboresha huduma kwa abiria wa SGR wa Dodoma na Morogoro ambayo ni miji inayohudumiwa kikamilifu na SGR kwa sasa na kampuni husika kufanya biashara ya huduma za usafirishaji, hali inayonufaisha pia serikali.

Kampuni ya Faima imesema kesho itaanza kutoa huduma rasmi kwa abiria wa Stesheni ya Morogoro na Dodoma.

Huduma hizi kwa mujibu wa taarifa ni kuwapeleka katika vituo mbalimbali abiria wa njia moja.

Mfano wa Dodoma, treni ikishusha abiria mabasi ya kampuni hiyo ambayo ni saba yatabeba abiria 472 na kuwapeleka katika vituo.

Vilevile kwa Stesheni ya Morogoro mabasi yatakuwa sita ya kawaida na moja la daraja la juu, watashushwa katika vituo vilivyoainishwa na gharama ya uchangiaji wa huduma hizo ni Sh 5,000 kwa kila abiria mmoja.

Sisi tunasema, tunaipongeza TRC kwa ubunifu huo wa huduma kwa abiria ambao kimsingi, uchangiaji wake ni kiwango rafiki ukilinganisha na umuhimu wa huduma kwa abiria.

Tunasema ni huduma muhimu kwa kuwa kwa asili yake, stesheni hizo zinaweza kuwa mbali na baadhi ya maeneo au vituo muhimu katika miji hiyo yenye abiria wengi.

Kimsingi, tunapongeza tukijua kwa dhati kuwa huduma hizo zitarahisisha usafiri kwa abiria na kupunguza usumbufu baada ya kushuka kwenye treni.

Si hivyo tu, bali pia tunaamini huduma hizo zinalenga kuongeza urahisi wa usafiri kwa abiria wa SGR kwa kuwaunganisha moja kwa moja kutoka stesheni hadi maeneo hayo bila usumbufu wa kutafuta usafiri wa ziada.

Pia tunapongeza kampuni hiyo ya kutoa huduma kwani inawahakikishia abiria huduma bora, salama na zenye viwango stahiki.

Kubwa zaidi ni kuwa, ratiba ya huduma hizo zitaendana na muda wa kuwasili na kuondoka kwa treni za SGR ili kurahisisha mwenendo wa safari.

Huu ni ubunifu unaotupa kila sababu ya kuipongeza TRC kwani si tu kurahisisha huduma kwa abiria, bali pia zinachangia kupunguza uhaba wa ajira nchini.

Sunday News, Sunday September 14, 2024
Pg 12



A traffic police officer observes traffic under the bridge along Kilwa Road, near Kurasini Junction, as daladala operators unlawfully stop in non-designated areas. (Photo by Venance Nestory)

Habari Leo, Jumapili Septemba 14, 2025 Pg 6




Madereva wa daladala wakiwa wameegesha magari chini ya daraja katika makutano ya Barabara ya Mandela na Kilwa, Dar es Salaam wakisubiria abiria katika eneo ambalo hawaruhusiwi kufanya hivyo kulingana na taratibu za usalama barabarani. (Picha na Venance Nestory).

Mwananchi, Jumapili, Septemba 14, 2025 pg 8

# Ni wakati sahihi wa mamlaka kuzidhibiti bajaji, bodaboda

Kwa muda mrefu, miji mingi nchini Tanzania imekuwa ikikabiliwa na changamoto kubwa ya uendeshaji holela wa vyombo vya usafiri, hususan pikipiki za kubeba abiria maarufu bodaboda na zile za magurudumu matatu zifahamikazo kama bajaji.

Licha ya mchango wake katika kutoa huduma ya usafirishaji ulio nafuu na haraka, usimamizi hafifu wa sekta hii umesababisha kero na madhara makubwa kwa jamii, zikiwamo ajali, usumbufu kwa watumiaji wengine wa barabara, na hata vifo.

Tukio la hivi karibuni jijini Moshi la dereva wa bajaji, Boniface Mtafya kufikishwa mahakamani na kuhukumiwa kwa kosa la kuiegesha katika eneo lisiloruhusiwa na kubeba abiria kupita kiasi, linafungua mjadala mpana zaidi kuhusu mustakabali wa nidhamu ya usafirishaji wa aina hii nchini.

Hukumu hiyo iliyoamriwa na Mahakama ya Wilaya na kuthibitishwa na Mahakama Kuu ni ishara kuwa sasa mamlaka zimeanza kuona uzito wa tatizo hili na kuwa linaweza kushughulikiwa na sheria zilizopo.

Hali ya sasa katika miji mingi, ikiwamo Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Kigoma, Iringa na mingine, ni ya wasiwasi. Bajaji na bodaboda wamegeuza barabara kama mali binafsi. Wanasimama popote wanapojisikia, katikati ya barabara au maeneo yenye msongamano mkubwa wa magari, ili kupakia abiria. Mara zote wenyewe huamua kuzipita taa nyekundu kana kwamba hakuna tatizo lolote. Tabia hii haileti tu usumbufu mkubwa kwa madereva wengine na watembea kwa miguu, bali pia inahatarisha maisha ya wote wanaotumia barabara wakiwamo wao wenyewe.

Takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) zinaonyesha wazi ukubwa wa tatizo: kati ya Januari na Desemba 2024, kulitokea ajali 383 za pikipiki Tanzania Bara, zikisababisha vifo vya watu 352. Idadi hii kubwa haiwezi kuachwa iendelee kana kwamba ni jambo la kawaida.

Sababu kubwa ya kuendelea kwa hali hii ni nidhamu ndogo miongoni mwa waendesha vyombo hivyo na usimamizi mbovu kutoka kwa mamlaka husika. Wengi wa madereva hawafuati masharti ya leseni zao, wengine hufanya kazi nje ya maeneo waliyosajiliwa, na baadhi huendesha bila mafunzo ya kutosha ya usalama barabarani.

Hali hii inachangia kuzorotesha hadhi ya usafiri mijini na kuongeza mzigo kwa vyombo vya usalama na sekta ya afya kutokana na majeruhi wa ajali na kwa jamii kuhudumia majeruhi na gharama za mazishi.

Ni wazi kuwa adhabu zilizopo sasa, ikiwamo faini ndogo ambazo hivi karibuni zimeshushwa hadi Sh10,000, hazina tija. Badala ya kuwa fundisho, zimekuwa zikihamasisha marudio ya makosa yale yale.

Inahitajika mapitio ya kina ya viwango vya faini na adhabu, sambamba na kuanzishwa kwa kanzi data ya kitaifa itakayohifadhi kumbukumbu za madereva wote waliopatikana na hatia. Mfumo huu utawezesha mamlaka kufuatilia wahalifu sugu na kuchukua hatua kali zaidi kwa wanaorudia makosa.

Aidha, usimamizi wa sekta hii unahitaji mabadiliko makubwa ya kimuundo. Latra, polisi na serikali za mitaa zinapaswa kushirikiana kwa karibu zaidi kudhibiti maeneo ya kuegesha na kuhakikisha kila dereva anafanya kazi kulingana na leseni yake.

Ni muhimu pia kuwekeza katika elimu endelevu ya usalama barabarani kwa madereva hawa, sambamba na kampeni za uelewa kwa wananchi kuhusu haki na wajibu wao wanapotumia huduma hizi.

Kwa mtazamo wa kijamii, bajaji na bodaboda si adui wa maendeleo, bali washirika muhimu iwapo wataendeshwa kwa nidhamu na udhibiti thabiti. Ni usafiri unaorahisisha maisha ya wananchi wengi, hususan mijini yenye misongamano. Lakini bila nidhamu, faida hizo hubadilika na kuwa mzigo kwa jamii.

Ni wakati sasa mamlaka husika zikaweka mkakati wa kitaifa wenye meno ya kudhibiti uendeshaji holela wa vyombo hivi. Nidhamu barabarani si hiari, bali ni sharti la kulinda maisha, mali na heshima ya nchi yetu.